

Maswali na Majibu

1. Je, Biblia inafundisha kwamba kuna kitu cha nguvu kisicho cha kawaida kinachotujaribu?
Hapana. Biblia haijawahi kusema hivyo.
2. Dhambi hutoka wapi?
Hutoka ndani ya mawazo yetu na mioyo yetu.
3. Jaribio hukua halafu itutie kwa dhambi namna gani?
Tunajaribiwa. Halafu tunaiacha ijaze mawazo yetu. Baadaye tunakubali na tunatenda dhambi.
4. Majaribu ni mbaya?
Hakuna makosa kujaribiwa lakini tusiiweka kwa mawazo. Ni makosa ikiwa tutaendelea kuiwazo halafu ikue.
5. Mbona wakati mwingine Biblia inazungumzia dhambi kana kwamba ni mtu?
Inatusaidia sisi tuelewe vile dhambi ina nguvu na danganyifu.
6. Neno shetani ina maana gani?
Kipingamizi – anayepinga mwenzake au ni adui.
7. Neno ibilisi ina maana gani?
Anayezungumza mabaya kwa wenzake au anashudia uongo.
8. Ina maana gani kusema kwamba Yesu aliharibu nguvu za ibilisi?
Ibilisi ni mfano wa dhambi. Yesu aliharibu nguvu za dhambi kwa kushinda dhambi halafu akapeana uhai wake usiokuwa na makosa kama dhabihu.
9. Ibilisi aliyemjaribu Yesu alikuwa nani?
Ni mafikira yaliyotoka ndani ya mawazo yake na moyo wake.
10. Nani ndiye mkuu na nguvu za milele ulimwengu kote? *Mungu*

Mistari ya kukariri

Yakobo 1:14 – 15 Waebrania 4:15 Isaya 45:5 – 6

Mazungumzo

Zungumzia mbona Biblia inatumia picha ya dhambi kama ni kitu cha nguvu kisicho cha kawaida. Ni vitu kama gani hutujaribu? Tunaweza kuzuia namna gani mawazo maovu yasikue ndani yetu?

Kuandika

Soma yakobo 1:14 – 15. Eleza vile majaribu hukua na iwe dhambi.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 48 Ibilisi na Shetani

**SOMA 1 Yohana 3:8; Waebrania 2:14; Marko 7:21 – 23;
Yeremia 17:9; Waebrania 4:15 Isaya 45:5 – 6**


SOMO

Biblia inaeleza mwanzo wa dhambi katika ulimwengu mzima. Mawazo kwamba kuna kiumbe kisichoonekana (ibilisi au shetani) kinachowajaribu watu au kinasababisha maovu hapa duniani ni uongo.

Biblia inatufunza kwamba dhambi hutoka ndani yetu sio eti mjaribu anatoka inje. Hii inamaanisha sisi wenyewe tuajibike kwa dhambi zetu. Tunatenda dhambi kwa sababu tunafurahia tunachotaka kufanya. Inakuwa ni rahisi sana kufanya haja zetu za hila kuliko kufuata njia za Mungu.

Biblia inafunza kwamba dhambi hutoka kwa mawazo yetu au mioyo zetu. Yesu alisema, “Kutoka **ndani, ndani ya mioyo** ya watu, hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tama mbaya, ukorofi, hila, ufishadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavuhuu uovu wote **unatoka ndani** na inamfanya kuwa najisi.” Yeremia alisema, “**Moyo** ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha.”

Yakobo 1:14 – 15 inaeleza vile majaribu hukua na iwe dhambi. “Kila mtu hujaribiwa wakati **tamaa yake mbaya huvutwa** na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.”



Tunajaribiwa na tamaa yetu wenyewe. Jaribio lenyewe si dhambi – hiyo ni hali ya kawaida. Inakuwa mbaya kama tunakubali hiyo tamaa ikue dhambi ndani ya mawazo zetu. Huwa tunafikiria saa zote juu ya hayo makosa tunayotaka kufanya. Hatufikirii vile Mungu anataka tufanye. Tukikubali hiyo tamaa ikue na itawale katika mawazo zetu, mwishowe tutafanya dhambi.

Katika Biblia neno ibilisi na shetani sinatumika kama mfano wa dhambi kwa binadamu. Wakati mwingine Biblia inazungumzia dhambi kama ni mtu. Inatumika kama mfano wa kupita uwezo wa binadamu ili tuelewe vile dhambi ni daganyifu sana. Jaribio la kukuelegeza dhambini inayotoka ndani ni ya nguvu na saa zingine inaonekana kama adui mbaya sana anayetufanya tufanye makosa.

Neno shetani inamaana ya kipingamizi – anayepinga mtu au ni adui wake. Mara nyingi inatumika kwa mtu wa kawaida anayepinga au ni adui. Wakati mwingine inatumika kwa mtu aliye mzuri. Yesu aliita Petro ‘Shetani’ alipojaribu kupinga Yesu asifanye mpenzi ya Mungu. (Mathayo 16:23). Kwa Hesabu 22:22, tunaambiwa juu ya nabii Balaamu, aliyekuwa anaenda kuwalaani Waisraeli. ‘Hasira ya Mungu iliwaka kwa sababu alienda, malaika wa Bwana akasimama barabarani kama kipingamizi (neno la asili ni shetani).’ Malaika alikuwa anapinga kitendo cha Balaamu. Malaika alikuwa anasaidia Balaamu lakini aliitwa shetani.

Petro na malaika hawakukuwa watu wabaya waliokuwa na uwezo. Shetani inamaanisha adui. Adui mkubwa wa watu ni dhambi iliyo ndani yake. Neno shetani kwa Agano Jipya linatumika kama picha ya dhambi. Linatumika kama mfano wa kitu kinachopinga Mungu.

Neno ibilisi linamaana ya mtu anayezungumza mabaya juu ya mtu au anayeshtaki mwingine kwa uongo. Neno ibilisi limetumika tu kwa Agano Jipya. Halijatajwa kwa Agano la Kale. Wakati mwingine neno ibilisi linatumika kwa watu wa kawaida wasio wazuri au wasemao uongo juu ya wenzao. k.m. 1 Timotheo 3:11.

Kama neno ‘shetani’, ibilisi linatumika kama mawazo ya kibinadamu yanayopinga mapenzi ya Mungu. Waebrania 2:14 inatusaidia kuelewa. Huu mstari unatwambia kwamba Yesu alikuja kama mwanadamu, akafa msalabani ili aharibu ibilisi. Watu wengi wanafikiri ibilisi ni kitu kisichokufa na kinajaribu watu kufanya maovu. Kwa hivyo Yesu kama mwanadamu angewezaje kuharibu hiyo ibilisi ya nguvu isiyo ya kawaida kwa kukufa msalabani? Hii haileti maana hata!

Waebrania 2:14 inasema kwa kifo chake Yesu ‘aliharibu yule aliyekuwa na nguvu ya kifo – yaani **ibilisi**.’ Linganisha huu mstari na Waebrania 9:26 inayosema, ‘Yesu amefunuliwa – kuzitangua **dhambi** kwa dhabihu ya nafsi yake.’

Hiyo mistari inazungumzia kitu kimoja. Nguvu ya dhambi au ibilisi aliharibiwa wakati Yesu alikufa kwa sababu tunaweza kusamehewa kupitia kwa dhabihu ya nafsi yake. Kwa hivyo ibilisi ni mfano wa dhambi. Yesu alishinda dhambi kupitia kwa yeye mwenyewe.

Dhambi na ibilisi ni kitu kimoja

Ibilisi ni adui kwa Mungu	Dhambi ni adui kwa Mungu
Ibilisi huwajaribu watu	Dhambi huwajaribu watu
Ibilisi anadanganya	Dhambi inadanganya
Ibilisi anasababisha kifo	Dhambi inasababisha kifo
Yesu alishinda ibilisi	Yesu alishinda dhambi

Ibilisi ni msukumo wa dhambi ndani ya hali ya ubinadamu

Watu wengine hawataki kukubali kwamba Yesu alijaribiwa kama sisi. Jaribio yenyewe si dhambi. Tukikubali vile tumejaribiwa, hiyo inakuwa dhambi. Waebrania 4:15 inatwambia kwamba Yesu anaweza kutuhurumia wakati tunashindana na majaribu kwa sababu yeye mwenyewe alijaribiwa sawasawa kama sisi – lakini hakushindwa na majaribu wala dhambi.

Yesu alijaribiwa na ibilisi. Alikuwa amepewa nguvu za Roho Mtakatifu baada ya ubatizo wake. Fahamu kwamba alikuwa Roho wa Mungu (sio wa ibilisi) ndiye alimpeleka nyikani kujaribiwa. Yesu alikuwa na kazi kubwa mno ya kufanya ya kufundisha watu na kupeana uhai wake msalabani. Alikuwa ashindane na dhambi ndani yake. Alitakiwa kushinda majaribu kwa kutumia nguvu za Mungu alizokuwa nazo. Alitakiwa ashinde majaribu kwa kutumia njia rahisi badala ya njia ngumu ya mateso na maumivu iliyoelekea msalabani. Majaribu ya Yesu ilitoka kwa mawazo yake na moyo wake. Lakini alishinda zote.

Mungu ni wa nguvu, na ana uwezo kwa ulimwengu wote. Yeye ndiye muumba na anayeweka kila kiumbe hai kwa nguvu zake. Hakuna uwezo mwingine anayeweza kubishana naye. Mungu anasema, “Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine, zaidi yangu mimi hapana Mungu ...ya kuwa hapana mwingine zaidi ya mimi; Mimi ni Bwana wala hapana mwingine”. Isaya 45:5 – 6).

- ◆ Biblia haijawahi kusema eti watu wanajaribiwa na kiumbe kingine kilichokiovu.
- ◆ Dhambi hutoka ndani ya mawazo yetu na mioyo yetu.
- ◆ Dhambi ni msukumo wa nguvu kwa maisha yetu, inayotujaribu tufanye maovu.
- ◆ Neno shetani inamaanisha kipingamizi – yule anayetuzuia au ni adui.
- ◆ Neno ibilisi inamaanisha yule anayezungumza mabaya juu ya mwingine au anayehukumu kwa uongo.
- ◆ Wakati mwingine maneno ibilisi na shetani, yanatumika kwa watu wa kawaida kama kwa Petro.
- ◆ Ibilisi na shetani yanatumika kama hali ya mfano wa kitu cha nguvu kisicho cha kawaida ndiyo itusaidie tuelewe kwamba dhambi ina nguvu na ni mdanganyifu